

HYBRID WATERMELON

“Aina mpya ya matikiti za mviringo mrefu”



SENTINEL

ONGOZO MFUPI WA KUPANDA	
Nambari ya mbegu kwa kila gramu	23 -27 kwa kila gramu
Idadi ya mbegu za kupandwa	Elfu 5 - 6 kwa ekari
Urefu unao pendekezwa wa shimo la kupanda	Sentimita 2 - 4
Kiwango cha joto cha kuota kwa mbegu	Sentigredi 16 - 35
Siku inazo chukuwa kuchipuzwa	5 - 10
Nafasi katika mraba (mche hadi mche)	Sentimita 90 - 100
Nafasi katikati ya mraba (mistari)	Sentimita 100 - 150
Kiwango cha joto cha kukuza mmea	Sentigredi 22- 30
Mazingara yanayopendeza ya kukuza mmea	Joto jingi, unyevunyevu kidogo, Mvua Kidogo, jua
Mazao yanayotarajiwa	Tani 45 - 50 kwa Ekari
Urefu wa mizizi ufaao	Sentimita 90 - 130
Udongo unaofaa	Udongo wa tifufufu-kichanga, inayo wezesha maji kupenyeza vizuri. Sio udongo wa mfinyanzi/clay
Kiwango cha pH mchangani	pH 5-6-8
Maji yanayohitajika kila juma	Milimita 20-30 wakati kukisubiriwa kukua kwa tunda
Kiwango cha joto katika ghala	Sentigredi 10-15
Wadudu	<i>Cutworm, Bollworm, Melon flies, Vithripi (Thrips), Mnyoo Fundo (Nematodes) na Aphids</i>
Maradhi ya fangasi/ukungu	Vimelea vya Fusari (<i>Fusarium</i>), Downy mildew, Ubwiri Poda (<i>Powdery mildew</i>), Anthracnose, Fruit Blotch na Gummy Stem Blight
Matatizo ya mashina au matawi ya mimea	Majani kusinyaa, Mwozo wa nja
Lishe ya mmea:	
Nitrojeni (N)	Kilo 120 - 150 za nitrojeni/hekta
Fosfori (P)	Kilo 60 - 75 za fosfori/hekta
Potasiam/Kali (K)	Kilo 100 - 150 za Potasiam/hekta

Kanusho: Matokeo ya mbegu zetu yaweza kuathiriwa na hali ya anga, mazingatio ya mkulima, magonjwa, wadudu na mengine mengi tusizoweza kuthibitii. Maelezo yoyote kuhusu mbegu zetu na matokeo yake, yawe kwenye mazungumzo au katika maandishi kutoka Monsanto na waajiriwa wake, yametolewa kwa wema lakini, yasichukuliwe kama neno la Monsanto kuhusu matokeo au ubora wa mbegu zetu katika eneo mkulima atakazozikua. Matokeo haya hutegemea hali ya anga na menginezo. Monsanto yajiondoa lawamani dhidi ya maelezo yaliomo

MONSANTO KENYA LTD, TUSKER MATTRESS HEAD OFFICE MOMBASA ROAD

P.O. Box 47686 00100, NAIROBI, KENYA.

Tel: 254 20 2060922/44/3574301/2/3/4, Fax: 254 20 823086/3574300

Mobile: 254 0722 205294/0722 205529/0733 600468 / 0733 629414

Web: www.monsantoafrica.com


Seminis
grow forward


MAELEZO KUHUSU MBEGU MPYA YA MATIKITI MAJI

PATA NEGRA F1

“Aina mpya ya tikiti maji ya mvingo yenye mazao na sifa nzuri”

Ubora wake

- Yenye mazao mazuri, na uwezo wa kukupa tani 46 kwa kila ekari
- Ni tamu sana na yenye wekundu wa kung'ara
- Inakomaa katika muda wa siku 100-120
- Ni mvingo na wenye rangi ya kijani kibichi na hutoa tunda lenye mizani kati ya kilo 7-10
- Mmea unaokua haraka na una mazao mazuri
- Iliyo zingukwa na nyama ngumu, nzuri, yenye kukuwezesha kusafirisha hadi sehemu za mbali
- Ina kinga dhidi ya ugonjwa wa mnyauko unaosababishwa na vimelea aina ya Fusari (*Fusarium wilt*)



SENTINEL F1

“Aina mpya ya matikiti za mvingo mrefu”

Ubora wake

- Zenye kuzaa sana hadi tani 50 kwa kila ekari
- Ni ndefu, iliyoshiba na yenye rangi milia
- Aina tamu, yenye wekundu uliokolea na nyama iliyo na maji mengi
- Yenye kutoa matunda ya kufanana na iliyo na uzani baina kilo 11 - 14
- Tunda lenye nyama nyingi na umbo inayokuwezesha kusafirisha masafa mrefu
- Ina kinga dhidi ya maradhi ya vimelea aina ya Fusari (*Fusarium wilt Race 1*)
- Inakua tayari katika muda wa siku 100 -120

KUKUZA MATIKITI

Hali ya anga inayo hitajika

- Inahitaji hali ya hewa yenye joto na mwangaza wa jua wa kutosha
- Kiwango kidogo cha unyevu kwa sababu unyevu mwingi unasababisha maradhi. Unyevunyevu mwingi unaadhiri ubora na utamu wa tunda.
- Kiwango cha joto kiwe baina ya sentigredi 18 hadi 38

Udongo unao hitajika

- Inastawi vizuri katika aina mbalimbali za udongo. Matikiti yanahitaji ardhi yenye rotuba ya kutosha na wenye kupitisha maji vizuri.

- Uzalishaji wa matikiti unaweza kuadhiriwa na maradhi ya vimelea ya Fusari (*Fusarium*). Wakulima wanahitajika kupanda mbegu zinazohimili magonjwa ama kuwa na mfumo wa mzunguko wa mimea kwa zamu katika kipindi cha miaka saba (*7-year crop rotation*).
- Kiwango cha uchachu (pH) kiwe baina ya of 5.0-6.8 ilikuiwezesha mimea kufyonza madini
- Limepigwa jembe vizuri ili kuvunja sehemu ngumu ya mchanga na kuwezesha maji kupenyeza vizuri.

Utumizi wa mbolea

- Kuna haja ya kuupima udongo ili kujua uchachu (pH) wake na kiwango cha madini
- Kuweka kiritubisho aina ya *lime* kunaongeza kiwango cha uchachu (pH) mchangani na kuzuia maradhi ya mimea kama mwozo wa nja (*Blossom-end Rot*).
- Nitrogeni ina nyunyizwa mara mbili; wakati mmea una matawi kati ya 2 na 4 na pia sehemu inayobeba matunda inapoanza kutambaa.

Nafasi katikati ya mimea

- Ukubwa wa tunda unaohitajika ndio utakao eleza nafasi inayopaswa kuachwa katikati ya mimea. Nafasi kati ya sentimita 100 kwa 150 ndio bora zaidi.
- Ekari moja inahitaji mbegu 5,000.
- Mimea zaidi inaweza kupandwa ikiwa unyunyizia maji ni kwa mifereji na dripu (*drip irrigation*).

Maua na uchavushaji

- Uchavushaji ni muhimu. Weka mzinga wa nyuki ili kuhakikisha kuwa uchavushaji unafanyika.
- Njia zinazotumika kuzuia wadudu zitekelezwe kwa njia itakayo wahifadhi nyuki
- Inastahili kuwe na unyevu kiasi wakati wa maua na matunda

Jinsi ya kuzuia wadudu na magonjwa

- Wadudu wanao vama matikiti, melon fly na aphids ndio fishio kubwa katika kuvuna matikiti.

Tumia madawa yaliyo sajiliwa kupigana na wadudu hawa.

- Maradhi ya fangasi kama Alternaria, Fusarium, Antrachnose na ubwiri poda (*Powdery Mildews*) ni makali lakini yanaweza kukabiliwa kwa kutumia madawa ya *Fungicide* na kupanda mbegu yenye kuhimili maradhi.
- Magugu yaendeleo kungo'lewa, angalia usiharibu mizizi ya mimea.

Mavuno na kumudu

- Matikiti maji huvunwa yakiwa karibu sana na kuiva. Huu ni wakati ambapo sehemu ya juu ya tunda inayo gusa mchanga ina rangi ya samli/njano au sehemu inayo beba tunda inapoanza kusinyaa.
- Sehemu inayobeba ua inakatwa kuizua kukwaruza ngozi ya tunda ambayo inaweza kusababisha maradhi mengine.
- Matikiti yana hatari ya kupasuka wakati au baada ya kuvuna ikiwa mkulima atakosa kuzimudu vizuri
- Matikiti hayafai kurushwa wakati wa kuvunwa, wala kukanyagwa au kurundikwa zaidi.